

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



18 MEI, 2017



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 18 MEI, 2017


**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**III. MASWALI:**



**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**229. MHESHIMIWA MWANTAKAJE HAJI JUMA (BUBUBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na wimbi la Mabweni na hata Shule kuungua moto, hususan Tanzania Bara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hiyo.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

### **230. MHESHIMIWA KHAMIS MTUMWA ALI (KIWENGWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Taasisi za Muungano zinafanyiwa ukaguzi na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:-

Je, ni mara ngapi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeshirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukagua Taasisi za Ubalozi zilizo nje ya Nchi.

## **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **231. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Tanzania imesajili michezo kadhaa ambayo huingia kwenye medani ya Taifa kiushindani lakini kote huwa ni mashamba yanayozaa visingizio:-

(a) Je, Serikali haioni haja sasa ya kujipinda katika michezo michache kiushindani Kimataifa;

(b) Je, kama kukiwa na uamuzi huo inaweza kuwa ni michezo ipi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

**232. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Sera ya Elimu ya mwaka 2014 inaeleza wazi kuhusu Mitaala na utaratibu wa masomo katika Elimu ya Msingi (Kidato cha 1 - 4) na inasema Watoto wa Kidato cha 1-2 watasoma masomo yote ya Sayansi na wanapoingia Kidato cha 3 watachagua masomo wayatakayo kutokana na uwezo wao:-

- (a) Je, Waziri alipata wapi mamlaka ya kutangaza kuwa Vijana wote wa Elimu ya Msingi hadi Kidato cha 4 kusoma masomo yote ya Sayansi;
- (b) Je, kuna utafiti gani uliofanyika na matokeo kuonyesha haja ya Vijana wote kusoma Sayansi yaani kemia na fizikia.

## **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

### **233. MHESHIMIWA OTHMAN OMAR HAJI (GANDO):**

Atamuuliza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Moja kati ya maeneo yaliyomo kwenye Mkataba wa Ushirikiano baina ya Tanzania na Cuba (1986) ni pamoja na kuimarisha Sekta ya Afya:-

Je, ni kwa kiasi gani Tanzania imefaidika na utekelezaji wa Mkataba huo katika Sekta ya Afya.

### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA  
UWEKEZAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
18 MEI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**